

MBEGU ZA DARAJA LA KUAZIMIWA UBORA NI NINI?

Mfumo wa mbegu za daraja la kuazimiwa ubora (QDS) ni sehemu ya mfumo rasmi ya mbegu na pia hudhibiti ubora na usafi wa mbegu. QDS haina masharti makali na hutumia rasilimali chache kuliko mfumo rasmi ya udhibiti wa ubora wa mbegu. QDS inalenga kusambaza mbegu zilizoboreshwa kwa wakulima wadogo na huwahusisha katika uzalishaji wa mbegu.



MANUFAA YA QDS

- 1 Wakulima wanaweza kupata mbegu za QDS kwa sababu zinapatikana kwa urahisi, zinaaminika na ni bei nafuu kuliko mbegu zilizothibitishwa kikamilifu.
- 1 QDS inakubaliwa kwa haraka katika maeneo ambayo inazalishwa.
- 1 Wakulima wanaruhusiwa kuhifadhi na kutumia tena QDS kwa misimu 3 hadi 4.
- 1 Wakulima wanaweza kuuza na kubadilishana QDS miongoni mwao.
- 1 Mfumo wa QDS una manufaa sawia kwa wakulima wa kiume na wa kike wanaozalisha mbegu zilizoboreshwa.
- 1 Mfumo wa QDS inatoa fursa nzuri ya ajira kwa wakulima wanaozalisha mbegu zilizoboreshwa.

CHANGAMOTO ZA QDS

- 1 Wakati mwingine wakulima wanapokea msaada finyu kutoka kwa serikali na wadau wengine kuhusiana na mafunzo ya uzalishaji wa QDS.
- 1 Kuna ufikiaji wenye kikomo kwa mbegu za msingi kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu.
- 1 Wakulima wengi hawafahamu kuhusu uzalishaji na matumizi ya QDS.
- 1 Wakati mwingine wakulima wanakosa kuzifikia rasilimali fedha ili kuendeleza biashara yao ya uzalishaji wa mbegu.
- 1 Mara nyingine serikali inadhibiti operesheni za QDS katika eneo dogo la kijiografia, ili kulinda maslahi ya makampuni binafsi ya mbegu.



african centre for biodiversity